JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS–MIPANGO NA UWEKEZAJI

HOTUBA YA MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI, AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2024/25



NOVEMBA, 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

HOTUBA YA MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2024/2025

DODOMA, JUMATATU 06 NOVEMBA 2023

HOTUBA YA MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2024/2025

DODOMA, JUMATATU 06 NOVEMBA 2023

I: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa kuzingatia Kanuni ya 113 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2024/2025.
2. ***Mheshimiwa Spika,*** Awali ya yote, na kwa namna ya pekee, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua nimsaidie kazi katika nafasi hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji. Kupitia Bunge lako tukufu, ninamuahidi, Mheshimiwa Rais, utumishi wenye weledi, maarifa, bidii na utiifu kwake, serikali yake na kwa Chama Cha Mapinduzi. Aidha, ninatumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutunukiwa Digrii ya Heshima ya udaktari wa Falsafa kutoka Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru mnamo tarehe 10 Oktoba 2023. Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru ni moja ya vyuo vikuu bora nchini India. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kiongozi wa pili katika nchi yetu kutunukiwa digrii hii baada ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyetunukiwa digrii kama hiyo Mwaka 1985. Gazeti la The Citizen lilieleza kuwa Rais Samia ametunukiwa digrii hiyo kwa "***kutambua mchango wake mkubwa katika kuleta mapinduzi katika sekta za elimu, uchumi, demokrasia na maendeleo ya wanawake***". Kwa mujibu wa mtandao wa CNBC18.com, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ni "***mwanamke wa kwanza kutunukiwa heshima hii na Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru***".

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kutumia nafasi hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa **Spika wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter-Parliamentary Union-IPU).** Ushindi wako ni ithibati kuwa weledi na umahiri wako kiuongozi unatambuliwa na kuthaminiwa ndani na nje ya Tanzania. Hongera sana Mheshimiwa Spika na Ahsante sana kwa kuheshimisha Tanzania. Ninakutakia kila la heri na mafanikio makubwa katika kuitumikia nafasi hiyo muhimu duniani.
4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philipo Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kazi zao njema katika kumshauri na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake, na kwa miongozo na maelekezo yao muhimu wanayotupa sisi wasaidizi wao katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Spika wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuiongoza Zanzibar na utekelezaji makini wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika upande wa Zanzibar.
5. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini (CCM) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi (CCM) kwa maoni na ushauri wakati wa vikao vya kamati. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25 ninayowasilisha katika Bunge hili leo.
6. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kumshukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Mipango kwa uchapaji kazi wao na ushirikiano wanaonipatia katika kuiongoza Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji na Taasisi zilizo chini yake.
7. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu,

Hazina na manaibu makatibu wakuu wa Wizara hii, kwa ushirikiano wao katika kuandaa Mpango huu.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninampongeza Mheshimiwa Bahati Ndingo kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi.
9. **Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yamezingatia maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, mpango ambao umetokana na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na mipango mingine ya kikanda.
10. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, mapendekezo haya yamezingatia kikamilifu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hotuba yake ya kwanza Bungeni aliyoitoa siku ya Alhamisi tarehe 22 Aprili 2021 alieleza kuwa "***Dira na muelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita itakuwa kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya***" (uk. 10). Aidha, mapendekezo yamezingatia falsafa ya uongozi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo ni ***4R*** (***Reconciliation, Resilience, Reform*** and ***Rebuilding***) yaani Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya.
11. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inawasilishwa katika sehemu kuu sita. *Sehemu ya Kwanza* ni huu Utangulizi. *Sehemu ya Pili* ni tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi duniani na tafsiri yake katika uchumi wetu. *Sehemu ya Tatu* ni tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi nchini. *Sehemu ya Nne* ni tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 na 2023/2024. *Sehemu ya Tano* ni Mapendekezo ya (maeneo na vipaumbele vitakavyozingatiwa katika) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025. *Sehemu ya Sita* ni Hitimisho.

II: MWENENDO WA UCHUMI DUNIANI

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na kwamba hali ya ukuaji wa uchumi duniani inaelekea kuanza kurejea katika hali ya kawaida, kwa ujumla uchumi wa dunia bado haujaimarika kikamilifu (incomplete recovery) kutokana na athari za ugonjwa wa UVIKO 19 (COVID-19). Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi Duniani (World Economic Outlook) ya Mwaka 2023[1] iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (International Monetary Fund-IMF), kasi ya ukuaji wa uchumi duniani ni ndogo, huku tofauti za kikanda zikiwa wazi. Kiwango cha ukuaji wa uchumi duniani kinatarajia kupungua kutoka asilimia 3.5 mwaka 2022 hadi asilimia 3.0 mwaka 2023 na hadi kufikia asilimia 2.9 mwaka 2024, ikiwa ni kiwango cha chini kihistoria katika kipindi cha miaka 19 (kati ya mwaka 2000 na 2019) ambapo kiwango cha chini cha wastani cha ukuaji wa uchumi duniani kilikuwa asilimia 3.8.
13. ***Mheshimiwa Spika,*** kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea na zenye uchumi mkubwa (advanced economies) kinatarajiwa kupungua kutoka asilimia 2.6 mwaka 2022 hadi asilimia 1.5 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 1.4 mwaka 2024. Ukanda huu unajumuisha nchi za Marekani, Japani, Uingereza, Kanada, Ujerumani, Ufaransa, Italia, Uhispania, na maeneo mengine ya Ulaya (eneo la Euro).
14. ***Mheshimiwa Spika,*** kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa ukanda wa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi (emerging markets and developing countries) kinakadiriwa kupungua kwa kiwango cha wastani wa kutoka asilimia 4.1 hadi asilimia 4.0 kwa mwaka 2023 na mwaka 2024. Ukanda huu unajumuisha nchi za China, India, Urusi, Brazili, Mexico, eneo la *Latin America* na *Carribbean*, Eneo la Mashariki ya Kati na Asia ya Kati, Nigeria, Afrika Kusini na Nchi za Kusini Mwa Jangwa la Sahara.
15. ***Mheshimiwa Spika,*** kasi ndogo na hata kupungua kwa kiwango cha ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea (advanced economies) katika kipindi husika kinatokana na uamuzi wa Marekani na baadhi ya nchi za Ulaya kupandisha kiwango cha riba katika Benki Kuu zao. Aidha, vita vinayoendelea kati ya Urusi na Ukraine vimeendelea kuyumbisha uchumi

[1] International Monetary Fund (IMF, 2023). Economic outlook: Navigating global divergences. Retrieved on 2023-10-21 from https://www.imf.org/en/Publications/WEO/Issues/2023/10/10/world-economic-outlook-october-2023

wa dunia, hususani katika kupandisha gharama za maisha na mfumuko wa bei za nishati na chakula katika nchi hizi. Mbali na athari za UVIKO - 19 na vita kati ya Urusi na Ukraine, kiwango cha ukuaji wa uchumi katika nchi za Asia kimeendelea kudorora kutokana na changamoto ya ujenzi wa nyumba unaoendelea nchini China ambapo baadhi ya makampuni makubwa na yanayotegemewa katika shughuli za ujenzi wa nyumba yamekumbwa na uhaba mkubwa wa mtaji. Hali hii imesababisha kampuni nyingi zinazojihusisha na ujenzi wa nyumba (real estate) kukumbwa na changamoto ya mitaji na hivyo kuanza kuondoa imani kwa wanunuzi wa nyumba nchini China.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatarajiwa kupungua kutoka asilimia 4.0 mwaka 2022 hadi asilimia 3.0 mwaka 2023 na kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatarajiwa kurejea katika asilimia 4.0 mwaka 2024. Mbali na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, kiwango kidogo cha ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kilisababishwa na kudorora kwa hali ya usalama kwa baadhi ya nchi katika ukanda huu. Kielelezo Na. 2 kinaonesha kwa kina hali ya uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kielelezo 1: *Hali ya Uchumi wa Dunia*



Chanzo: Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia, IMF, 2023.



Chanzo: Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia, IMF, 2023.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Taarifa ya IMF inaonesha kuwa kiwango cha uchumi kilikua kwa asilimia 5.3 mwaka 2022 na kinatarajiwa kukua hadi kufikia asilimia 5.4 kwa mwaka 2023. Kielelezo 3 kinaonesha hali ya ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Afrika Mashariki.



Chanzo: Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia, IMF, 2023.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO) ya Aprili 2023, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka kwa kiwango kikubwa na kufikia wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2021. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2021. Vilevile, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2021. Mwaka 2022, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulifikia wastani wa asilimia 14.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2021.
19. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 11.2 mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.6 mwaka 2021 na unatarajiwa kuongezeka na kufika asilimia 11.9 mwaka 2023. Mfumumko wa bei katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unaweza kutazamwa kwa namna mbili: viwango vya mfumuko wa bei kwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda viliendelea kuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8. Kwa upande mwingine, nchi za Burundi na Rwanda zilikuwa na viwango vikubwa vya mfumuko wa bei mwaka 2022 uliofikia asilimia 18.9 na 13.9 mtawalia.
20. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, mwelekeo wa uchumi duniani una tafsiri (implications) katika uchumi wa Taifa letu. Uchumi wa dunia unapodorora husababisha, pamoja na mambo mengine, kudorora kwa upatikanaji wa fedha za mikopo, kupanda kwa riba za mikopo, na uwezekano wa kupungua kwa misaada kutoka kwa nchi wahisani.

III: MWENENDO WA UCHUMI WA TAIFA

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2022 thamani halisi ya Pato la Taifa (GDP) kwa bei za Mwaka 2015 ilikuwa shilingi trilioni 141.9, ikilinganishwa na shilingi trilioni 135.5 Mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.5. Kwa mujibu wa Benki ya Tanzania (BoT), kiwango halisi cha ukuaji kilikuwa asilimia 4.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.9 mwaka 2021. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kinatarajiwa kuwa asilimia 5.2 mwaka 2023

na asilimia 6.1 mwaka 2024. Ukuaji huu unatokana na nchi kuendelea kukabaliana vyema na athari zilizosababishwa na UVIKO 19, pamoja na mikakati thabiti ya kukabiliana na athari za vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, ukuaji huu unatarajiwa kuchangiwa na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususani makaa ya mawe; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochagiza shughuli za kiuchumi; na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwezi Juni 2023[2], shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 4 ni pamoja na : kilimo (15.9%); ujenzi (15.5%); madini (11.9%); biashara na matengenezo (9.8%); na uzalishaji viwandani (9.0%).

Kielelezo 4: *Mchango wa Sekta katika Ukuaji wa Uchumi kwa Robo Mwaka Inayoishia Juni 2023 (%)*



Chanzo: Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Robo Mwaka Inayoishia Juni 2023.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka 2022, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2021. Katika kipindi kilichoishia Septemba 2023, mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 3.3

[2] Bank of Tanzania (2023). Economic bulletin for the quarter ending June 2023 (Volume 2, June 2023).

ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kwa ujumla, mfumuko wa bei nchini umeendelea kuwa ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia tatu (3%) hadi saba (7%). Hali hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma na kuongezeka kwa upatikanaji wa mazao ya chakula nchini.

24. **Mheshimiwa Spika,** *maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika Sura ya Kwanza ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025.*

25. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya muda mrefu inaonesha kuwa uchumi wa Tanzania umekuwa ukikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia sita kwa mwaka katika kipindi cha miaka 20 iliyopita kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 5. Aidha, uchumi wa Tanzania ulionesha hali kubwa ya ustahimilivu hata katika kipindi cha misukosuko mikubwa ya kiuchumi duniani, ikiwemo wakati wa janga la ugonjwa wa UVIKO - 19 na vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Ni katika hali hii shughuli za uchumi zimekuwa zikiongezeka katika maeneo na maisha halisi ya Watanzania.



Kielelezo 5*: Wastani wa Kiwango cha Ukuaji wa Uchumi Tanzania: 2000-2020*

26. Aidha, katika kipindi cha miaka 20 iliyopita aina ya bidhaa tunazouza nje na nchi tunazofanya nazo biashara zimebadilika sana. Miaka 20 iliyopita

tuliuza zaidi mazao ya kilimo wakati sasa mauzo yetu ya nje yanatawaliwa zaidi na mauzo ya madini. Aidha, miaka 20 iliyopita tuliuza zaidi bidhaa zetu katika masoko ya Ulaya, Marekani na Afrika, lakini kwa sasa tunauza zaidi katika masoko ya nchi za Asia (China, India, n.k.) na Mashariki ya Kati kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 6-9.



Kielelezo 6: Mauzo ya Bidhaa Mwaka 2000



Kielelezo 7: Mauzo ya Bidhaa Mwaka 2020



Kielelezo 8: Nchi ambazo Tanzania iliuza Bidhaa zake Mwaka 2000



Kielelezo 9: Nchi ambazo Tanzania iliuza Bidhaa zake Mwaka 2020

27. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, kama ambavyo Benki ya Dunia wameeleza katika taarifa yao ya Septemba 2023 kuhusu uchumi wa Tanzania (Tanzania Economic Update 2023), uchumi wa Tanzania umeendelea kuhimili vyema athari za UVIKO - 19 na changamoto zingine za dunia zilizojitokeza katika miaka mitatu iliyopita. Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Benki ya Dunia, pamoja na changamoto zilizojitokeza uchumi wetu

umeendelea kuimarika kutokana na sababu kuu tatu. Mosi, utekelezaji wa mageuzi makubwa yaliyolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi, sambamba na eneo la kwanza la kipaumbele katika ***Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26*** - "***Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi***". Pili, kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Tatu, kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani, pamoja na wadau wetu wa maendeleo.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinuia kiwango cha miasha ya watu wetu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mrefu na mfupi ijayo itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu ***unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unatengeneza utajiri na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi***. Ili kufikia azima hii, mkazo mahususi utawekwa katika sekta za uzalishaji ambazo zinahusisha watu wengi. Mkazo wa kipekee utawekwa katika ***kuchochea maendeleo kijamii na kiuchumi vijijini*** (rural socio-economic development).

IV: TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA YA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyokuwa kwa mipango iliyopita, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2022/2023 na wa Mwaka 2023/2024 ulizingatia vipaumbele vitano, ambavyo ni: *kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji na utoaji wa huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu,* na *kuendeleza raslimali watu*. Miradi na programu mbalimbali zilitekelezwa katika kufikia malengo haya.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji katika sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini hatua zifuatazo zimechukuliwa:

    i) Kuongeza matumizi ya mbolea kwa asilimia 46, kutoka tani 363,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 531,091 mwaka 2022/2023.

    ii) Kuongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 300,000 na hivyo kufikia hekta 800,000 za umwagiliaji kati ya hekta milioni 1.2 ambalo ni lengo lililowekwa katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano.

    iii) Kukamilisha ujenzi wa majosho 246 na ununuzi wa chanjo za mifugo milioni 696.4.

    iv) Kuanza kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hizo ni:

    i) Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani 20,402,014 mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19 katika kipindi cha mwaka mmoja. Hali hii imeimarisha hali ya usalama wa chakula nchini ambapo hali ya utoshelevu wa chakula imefikia asilimia 124 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 130 ifikapo mwaka 2025/2026.

    ii) Hali ya masoko ya mazao ya wakulima imeimarika ambapo Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (National Food Reserve Agency-NFRA) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) wamenunua jumla ya tani 62,558.584 za mazao mbalimbali kutoka kwa wakulima.

iii) Kuongezeka kwa fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini kutoka dola za kimarekani bilioni 3.1 mwaka 2021 hadi dola za kimarekani bilioni 3.4 mwaka 2022, na kuchangia asilimia 56 ya mauzo yote ya nje, ikilinganishwa na lengo la kuchangia asilimia 50.5 lililowekwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azima yake ya kuyaendeleza mema aliyoyakuta wakati anaingia madarakani, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo ya ujenzi wa miundo mbinu nchini, ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR). Ujenzi wa reli hii utakapokamilika utakuwa moja ya nyenzo kubwa katika Sekta ya uchukuzi nchini Tanzania itakayotoa mchango katika Sekta ya Uchukuzi kwa kuitumia fursa ya kijiografia iliyopo. Mradi huu unagharimu jumla ya shilingi trilioni 23.3 unahusisha awamu mbili. Awamu ya kwanza ni ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye vipande (lots) vitano: Kipande cha 1: Dar es Salaam -Morogoro (KM 300); Kipande cha 2: Morogoro – Makutupora (KM 422); Kipande cha 3: Makutupora – Tabora (KM 368); Kipande cha 4: Tabora – Isaka (KM 165); na Kipande cha 5: Isaka – Mwanza (KM 341). Awamu ya pili inahusu ujenzi wa reli kutoka Tabora hadi Karema yenye urefu wa KM 1,010 na inajengwa katika vipande (lots) vitatu: Kipande cha 1: Tabora – Kigoma (KM 411); Kipande cha 2: Uvinza – Musongati – Gitega (KM 282); na Kipande cha 3: Kaliua – Mpanda -Karema (KM 317).
33. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Mwezi Aprili 2021, wakati serikali ya awamu ya sita inaingia madarakani, ujenzi wa reli hii ulikuwa katika vipande viwili vya Dar es Salaam – Morogoro (83.5%) na Morogoro – Makutupora (57.57%) na malipo yenye thamani ya shilingi trilioni 4.4 (kati ya shilingi trilioni 7.4) yalikuwa yamefanyika. Hadi Septemba 2023, ujenzi wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 98.60 na kipande cha pili umefikia asilimia 95.41 na malipo yamefikia shilingi trilioni 6.3. Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imeanza ujenzi wa vipande vingine vipya vitano: Makutupora – Tabora ambao (12.32%); Isaka – Mwanza (37.20%); Tabora – Isaka (4.10%); Tabora – Kigoma (KM 506) na Uvinza – Gitega (KM 367) ambao upo katika hatua ya manunuzi.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi mingine ya kielelezo imeainishwa kwa kina katika Sura ya Pili ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo.
35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchochea uchumi shindani na shirikishi, pamoja na hatua zingine, Serikali ilikamilisha mchakato wa kupata mwekezaji wa kuwekeza, kuendeleza na kuendesha Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi (IGA) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mamlaka ya Falme ya Dubai mwezi Juni 2023, hatimaye siku ya Jumapili tarehe 22 Oktoba 2023 mikataba mitatu ya utekelezaji wa miradi katika kuwekeza na kuendesha Gati za 0-3 na Gati za 4-7 zilisainiwa katika ya TPA na Kampuni ya DP World. Kufuatia hatua hii, Serikali inatarajia kuwa mapinduzi makubwa ya kiuwekezaji, kiuendelezaji na kiutendaji yatatokea katika Bandari ya Dar es Salaam katika siku chache zijazo.
36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza biashara na uwekezaji, pamoja na hatua zingine, Serikali iliendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji. Kati ya Juni 2021 na Septemba 2023 jumla ya miradi 883 imesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji ikiwa na thamani ya dola za kimarekani milioni 12,154 ambayo imezalisha ajira 160,107.
37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kiwango cha mauzo ya bidhaa za viwandani (manufacturing goods) kiliongezeka kwa asilimia 20.8, kutoka dola za kimarekani milioni 1,109.3 mwaka 2021 na kufikia dola za kimarekani milioni 1,340.5 mwaka 2022 na baadaye kufikia dola za kimarekani milioni 1,401.2 mwaka 2023[3].
38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchochea maendeleo ya watu, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi ilifikia asilimia 108.5 mwaka 2022, ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 100 mwaka 2025/26. Aidha, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa sekondari (Kidato cha I-IV) kimeongezeka kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 48.2 mwaka 2022, ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia asilimia 48 mwaka 2025/26. Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari (Kidato V - VI)

[3] BoT Monthly Economic Update, September 2023, Available at https://www.bot.go.tz/Publications/Filter/2

kimeongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2021 hadi asilimia 7.6 mwaka 2022 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la asilimia 10 mwaka 2025.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022[4]; na Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.
40. ***Mheshimiwa Spika***, katika sekta ya maji, utekelezaji wa miradi 630 yenye vituo 6,553 vya kuchotea maji vinavyonufaisha wananchi wapatao 4,393,274 kwenye vijiji 1,390 umekamilika. Kiwango cha wananchi wanaopata maji safi na salama kimefikia asilimia 88.6 mijini na asilimia 78 vijijini.
41. Katika **sekta za huduma**, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii 1,711,625 mwaka 2021 kufikia watalii 3,818,080 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 123.1 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la watalii 5,000,000 mwaka 2025; kuongezeka kwa mapato ya utalii kutoka dola za kimarekani bilioni 1.31 mwaka 2021 kufikia dola za kimarekani bilioni 2.53 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 93.1 ikiwa ni jitihada za kufikia lengo la dola bilioni 6.0 mwaka 2025.
42. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio haya ni matokeo ya maamuzi sahihi ya Serikali ya kupanga kwa muda mrefu, wa kati na mfupi, misingi thabiti ya uchumi na utekelezaji wa sera madhubuti za uchumi jumla, jitihada za makusudi za Serikali kujenga mazingira wezeshi na rafiki ili kuchochea shughuli za kiuchumi na maendeleo nchini pamoja na ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo katika utekelezaji wa ajenda ya maendeleo. Maelezo ya kina kuhusu mafanikio na hatua za utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2022/23 na robo ya kwanza ya mwaka 2023/24 yapo kwenye Sura ya Pili ya Kiitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo

[4] Ministry of Health (MoH) [Tanzania Mainland], Ministry of Health (MoH) [Zanzibar], National Bureau of Statistics (NBS), Office of the Chief Government Statistician (OCGS), and ICF. 2022. *Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey 2022 Final Report.* Dodoma, Tanzania, and Rockville, Maryland, USA: MoH, NBS, OCGS, and ICF.

V: MAPENDEKEZO YA MWELEKEO NA MAENEO YA KIPAUMBELE KATIKA MPANGO WA MAENDELEO YA TAIFA WA MWAKA 2024/2025

43. ***Mheshimiwa Spika,*** tathimini ya utekelezaji wa mpango wa muda mfupi wa maendeleo wa taifa inaonesha kuwa hatua kubwa imefikiwa katika utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya maendeleo, na mafanikio mengi yamepatikana katika sekta mbalimbali. Mafanikio haya ni pamoja na maendeleo mazuri ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati, ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na Bwawa la Mwalimu Nyerere. Aidha, katika kipindi cha taarifa hii, matumizi ya mbegu bora, mbolea na kilimo cha umwagiliaji yameongezeka, hali iliyosababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali. Vilevile, mauzo nje ya nchi yameendelea kuongezeka na huduma za jamii zimeendelea kuimarika, ikiwa ni pamoja na elimu, afya, na maji.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** tathimini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa katika kipindi cha muda mrefu inaonesha kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kukua mfufulizo kwa wastani wa asilimia sita katika kipindi cha miaka ishirini na katika kipindi chote hicho mfumuko wa bei umeendelea kustahamilika. Aidha, mauzo ya nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 975 Mwaka 2000 hadi Dola za Kimarekani bilioni 5.91 Mwaka 2020. Hata hivyo, katika kipindi chote hiki mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi yametawaliwa na usafirishaji wa mali ghafi bila kuongezea thamani. Kwa sababu hii, kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa haiendani na kasi ya kupunguza umaskini na kuzalisha ajira, hususani katika maeneo ya vijijini.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia usuli huo, ninapendekeza kuwa shabaha Kuu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025 na miaka ijayo iwe ni ***kuchochea kasi ya ukuaji uchumi ambao ni jumuishi, unaopunguza umaskini, unaozalisha ajira kwa wingi, unaotengeneza utajiri, na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi***. Katika kufikia shabaha hii, msukumo utawekwa katika kuongeza tija ya uzalishaji na uongezaji thamani katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini; kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo

katika ngazi zote; kuongeza na kuimarisha matumizi zaidi ya teknolojia, hususan teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA); kuongeza uzalishaji viwandani; na kuimarisha huduma bora za jamii kwa wote.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwaka 2024/2025 na kipindi cha muda wa kati ni kama ifuatavyo:

i) Pato la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2024;

ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 7.0 katika kipindi cha muda wa kati;

iii) Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 12.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/25 kutoka uwiano halisi wa asilimia 11.9 uliofikiwa mwaka 2022/23;

iv) Kudhibiti ukuaji wa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.2 ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025 kutoka matarajio ya asilimia 2.7 ya mwaka 2023/2024;

v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

vi) Kupunguza nakisi kwenye urari wa biashara na huduma kwa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Malengo ya jumla ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 ni:

i) Kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano iliyopita.

ii) Kuendelea na juhudi za kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula nchini kwa kuendelea kuongeza matumizi ya mbolea, mbegu bora na kilimo cha umwagiliaji.

iii) Kuongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa (pamoja na huduma) nje ya nchi kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini.

iv) Kuweka mkazo wa pekee katika kuongeza thamani katika mazao yanayozalishwa kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini

v) Kuendelea kuongeza, kuboresha na kuimarisha ubora wa huduma za jamii, ikiwa ni pamoja na elimu, afya, maji na umeme.

vi) Kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga, na majini, na utunzaji endelevu wa mazingira; na

vii) Kujielekeza kwenye kufungua fursa katika sekta ya madini ya kimkakati (strategic minerals), uvuvi wa bahari kuu (deep sea fishing), uchumi wa kijani (green economy), na uchumi wa kidigitali (digital economy). Maeneo hayo matatu ni maeneo yanayokamata kasi duniani kwa sasa na ambayo kwa upande wetu hatujavuna ipasavyo.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** izingatiwe kuwa wananchi wengi nchini (65.1% ya idadi ya watu wote Tanzania[5]), wanaishi vijijini na kwamba shughuli nyingi za uzalishaji zinategemea kilimo. Aidha, sekta ya kilimo imeajiri asilimia 61 ya nguvu kazi, na kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi vijijini haiendi sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi mijini, na kwa kuwa ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani unategemea malighafi kutoka maeneo ya vijijini. Izingatiwe pia kwamba mifumo ya ugharimiaji wa shughuli za kiuchumi haishikamani na shughuli za kilimo vijijini (ambapo mikopo yote ya kibiashara nchini ni shilingi trilioni 22, wakati mikopo inayokwenda katika sekta ya kilimo ni 7% pekee). Hivyo basi, ninapendekeza kuwa katika mipango yetu ijayo ya maendeleo tuweke mkazo maalum katika kuhakikisha kuwa uchumi wa vijijini unakuwa sehemu muhimu ya uchumi wa taifa. Katika kuchochea na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini (rural socio-economic development) ninapendekeza kuchukua hatua saba zifuatazo:

i) Kuendelea kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwapatia wakulima wadogo (small scale farmers) mbegu bora na mbolea kwa bei ya ruzuku, na kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji.

ii) Kuweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani (primary processing) katika sekta za kimkakati, zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu. Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali (*semi-processed)*. Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Katika hatua hii,

[5] Wizara ya Fedha na Mipango (2023). Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2022 (Juni 2023).

tutahitaji kulipanga upya shirika la viwanda vidogo nchini (SIDO).

iii) Kuendelea kupanua na kuboresha miundombinu ya huduma za afya, elimu, maji, na umeme.

iv) Kuhakikisha kuwa angalau asilimia 30 ya wananchi vijijini wanakuwa na bima ya afya ifikapo Mwaka 2025.

v) Kuweka mkazo wa pekee katika kuimarisha ubora wa elimu, hususani katika kuhakikisha kuwa shule za vijijini zina walimu wa kutosha na kuunganishwa katika miundombinu ya kidigitali.

vi) Kwa kuzingatia umuhimu wa dijitali (digitalisation) katika kuleta mapinduzi ya uchumi vijijini, ninapendekeza kujenga mfumo wa dijitali vijijini (rural broad band) ili kuwaunganisha wananchi vijijini katika uchumi wa taifa na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, hatua hii itaiwezesha serikali kuwa karibu zaidi na wananchi, kusaidia katika mapambano ya rushwa, kuimarisha demokrasia na utawala bora.

vii) Kupitia upya sera za fedha, sheria na kanuni zinazosimamia mikopo kwa lengo la kuzisukuma taasisi za kifedha kuelekeza mikopo katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, na wachimbaji wadogo wa madini.

49. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka ujao, serikali itaweka mkazo katika kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza na kuimarisha ujazo wa fedha za kigeni. Ili kufikia azima hii, njia sahihi na endelevu ni kuhakikisha kuwa tunabadili mwelekeo kutoka kuuza bidhaa ghafi kwenda kuuza bidhaa zilizoongezwa thamani. Kwa kuzingatia hali ya ushindani duniani katika kuvutia uwekezaji, ninapendekeza kuchukua hatua zifuatazo katika kuvutia uwekezaji wa kimkakati katika uongezaji wa thamani wa mazao mbalimbali:

i) Kuweka mkakati wa kulenga masoko makubwa ya nje ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa kwa tija na ushindani kwa lengo la kuimarisha uwezo wetu wa kuuza nje (export led economy). Katika kufikia azima hii, tutafanya uchambuzi wa kina ili kuyabaini na kuyaelewa masoko haya ili kujua kwa dhati tunazalisha kwa ajili ya nani na kwa kuzingatia malengo yetu ya muda mrefu.

ii) Kwa kutambua nafasi ya uzalishaji wa nguo na mavazi katika kuzalisha ajira na umuhimu wa zao la pamba nchini katika maisha ya wananchi wetu, tutatoa msukumo wa pekee katika kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa viwanda

vya nguo. Aidha, kwa kutambua kwamba soko la nguo na mavazi ni soko lenye ushindani mkubwa duniani likitawaliwa na majina maarufu katika soko (*brands*) zilizokomaa na kudumu katika soko kwa miaka mingi, na kwa kutumia fursa ya wawekezaji wengi wa nguo na mavazi kuanza kukimbilia Afrika kwa sasa, tutaweka mazingira maalum kwa lengo la kuvutia kampuni zenye majina maarufu (*brands*) kushirikiana na wazalishaji wa ndani kuwekeza nchini katika kujenga viwanda vya nguo na mavazi.

iii) Kuanzisha Mtaa wa Sayansi, Teknolojia na Digitali (Science, Technology and Industrial Park) kwa ajili ya kuchochea na kuibua ubunifu na ugunduzi unaohitajika katika mapinduzi ya nne ya viwanda (fourth industrial revolution)

iv) Kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya nje, na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (*critical raw materials*) katika kutimiza azima ya dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira, tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini, hususani katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo.

v) Kuweka mkazo katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi, pamoja na ile inayoiwezesha nchi kutumia fursa za wakati (*opportunity of time*), ikiwemo:

i) Kuhakikisha kuwa mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe, chuma na madini adimu (critical minerals) katika eneo la Liganga na Mchuma unaanza kutekelezwa.

ii) Kuhakikisha kuwa nchi inaimarisha matumizi ya gesi (CNG) katika uendeshaji wa magari ili kuanza kupunguza utegemezi wa mafuta ya kuagiza nje ya nchi.

iii) Kuweka msukumo maalum katika miradi ya kuzalisha nishati ili kukabiliana kikamilifu na ongezeko la mahitaji ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo kukamilisha miradi ya umeme ya Bwawa la Mwalimu Nyerere na Kinyerezi.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio ya utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo umejengwa katika **nguzo kumi** zifuatazo:

i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi, katika nchi jirani na duniani kwa ujumla

ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini

iii) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini

iv) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara. Katika kutekeleza hili, tutahakikisha kuwa serikali inaendelea kujitoa katika kutekeleza huduma na miradi ambayo sekta binafsi inaweza kutekeleza kwa ufanisi zaidi ama kwa uwekezaji wa kawaida au kwa utaratibu wa ubia. Lengo ni kuhakikisha kuwa raslimali za serikali zinaelekezwa kwenye maeneo ambayo, kwa asili yake, sekta binafsi haiwezi kutekeleza kwa ufanisi au, pamoja na umuhimu wake, yanaweza yakawa hayana tija kibiashara.

v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko)

vi) Kuwa na raslimali watu wa kutosha na bora inayokidhi matakwa ya wakati ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu

vii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma

viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, hususani kwa wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wakati wa ndani

ix) Kuongeza tija ya uzalishaji (labour productivity) miongoni mwa watumishi wa umma na wafanyakazi kwa ujumla

x) Kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mambo tuliyopanga.

VI: HITIMISHO

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapohitimisha, ninaomba kusisitiza mambo matatu. Mosi, ni umuhimu wa kupanga vipaumbele vyetu vyema. Suala hili pia liliwahi kusisitizwa na Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika hotuba zake. Akihutubia Mkutano Mkuu wa TANU tarehe 28 Mei 1969, ambao ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo, pamoja na mambo mengine, Mwalimu alielezea umuhimu wa kuchagua katika kupanga, akisema: *"**Kupanga ni Kuchagua**. Kuweka Mpango maana yake ni kuamua jinsi ya kutumia raslimali iliyo haba; maana yake ni kuchagua kutimiza baadhi tu ya shughuli nyingi, na zote nzuri, kwa sababu haiwezekani kutimizwa zote mara moja. Katika hali zao mbalimbali, kila nchi ulimwenguni ina kikomo cha raslimali inayoweza kuitumia; na ikitumia raslimali nyingi zaidi katika shughuli moja, basi italazimika kupunguza raslimali itakayotumika katika shughuli nyingine" (uk. 3-4).*
52. ***Mheshimiwa Spika,*** ni wazi kuwa sisi kama nchi tuna mahitaji mengi lakini raslimali tulizo nazo zina kikomo. Kwa sababu hii tunawajibika kuchagua tufanye lipi leo na lipi tulifanye baadaye. Hii ndiyo maana ya kupanga. ***Kupanga ni Kuchagua***. Katika kupanga tutazingatia vipaumbele vya kimkakati kwa kuzingatia dunia inataka nini na sisi tunaweza kutoa nini.
53. ***Mheshimiwa Spika,*** Jambo la pili ni umuhimu wa kujenga maridhiano (consensus) ya kitaifa katika mipango tunayopanga. Maendeleo ni mchakato endelevu wenye kushirikisha wadau wote katika nchi. Tunachopendekeza hapa ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa, sio Mpango wa Serikali. Hivyo ni muhimu kuwa na maridhiano ya kitaifa kuhusu mwelekeo wetu kisera ili sote tushirikiane katika kujenga Tanzania tunayoitaka.
54. ***Mheshimiwa Spika,*** jambo la tatu ni umuhimu wa kuwa na watu makini, wenye weledi na uzalendo katika utumishi wa umma. Suala hili la kuweka kipaumbele kwa rasilimaliwatu limekuwa likitiliwa msisitizo na viongozi mbalimbali ulimwenguni. **Lee Kuan Yew** aliyekuwa Waziri Mkuu nchini Singapore anayeaminika kuwa ndiye kiongozi aliyeleta mapinduzi makubwa

ya kiuchumi nchini Singapore. Lee anaamini kuwa kitu cha kwanza kinachohitajika katika nchi kuendelea ni watu wazuri ndani ya serikali. Akihutubia Bunge la Singapore tarehe 1 Novemba 1994 kuhusu mapendekezo ya mishahara kwa mawaziri na akielezea umuhimu wa kuwa na viongozi wazuri serikalini alisema:

> *"My experience in Asia has led me to a different conclusion. To get good government, you must have good men [and women] in charge of government. I have observed in the last 40 years that even with a poor system of government, but with good strong men [and women] in charge, people get passable government with decent progress[6]".*

55. ***Mheshimiwa Spika,*** anachokisema Lee ni kuwa uwepo wa mfumo na taasisi nzuri ni muhimu na inasaidia. Lakini muhimu zaidi ni kuwa na watu wazuri katika kuendesha mifumo na taasisi za serikali. Ndio kusema hatuwezi kuwa na serikali nzuri bila kuwa na watu wazuri wanaoendesha serikali. Utawala bora unahitaji serikali bora na ili kuwa na serikali bora tunahitaji watu na viongozi bora wanaoendesha serikali. Kwa kuzingatia hili, Serikali itaendelea kuwekeza katika kuwa na idadi sahihi ya watumishi wa umma wenye weledi, maadili na uzalendo kwa nchi yao.
56. ***Mheshimiwa Spika,*** sisi kama nchi tunaye kiongozi mkuu wa nchi makini aliyeonesha weledi na kuthibitisha uadilifu na uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yake. Zaidi ya yote amethibitisha kuwa kiongozi muungwana na mpenda haki. Kupitia falsafa yake ya 4R, amejenga maridhiano mapana ya kijamii na kisiasa na kuweka mazingira sawia ya kufanya siasa kwa vyama vyote nchini (R1 =*Reconciliation*); ametoa uhuru wa kutosha wa kutoa maoni bila woga wala vitisho huku akionesha ustahimilivu wa hali ya juu (*R2=Resilience*). Kiongozi wetu ameleta mageuzi makubwa katika kuweka mazingira bora ya biashara na uwekezaji (R3 = Reform). Amefufua sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini na kuwapa matumaini mapya mamilioni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wadogo wa madini. Hakika anaijenga upya nchi yetu (R4 =Rebuilding) na kupitia uongozi wake, Serikali na nchi yetu ipo salama. Naam, hapa ninamzungumzia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

---

[6] Kwang, H.F., Fernandez, W., & Ten, S. (1998). *Lee Kuan Yew: The man and his ideas*. Singapore Press Holding (p.89).

57. **Mheshimiwa Spika,** ““***Kuzeeka peke yake ndio inaweza kutokea bila kupanga***”. Lakini maendeleo ya kweli yatatokana na mipango mizuri na nidhamu ya utekelezaji wa mipango hiyo. Akihutubia katika Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Dodoma, tarehe 25 Agosti 2004, Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin William Mkapa, alisisitiza umuhimu wa mipango mizuri kwa kusema: “***Kuongoza ni kupanga kwanza. Mipango mizuri huleta maamuzi mazuri kimkakati na kiutendaji”***. Waheshimiwa Wabunge, sisi ndio viongozi wa nchi hii. Tuna wajibu wa kupanga na kupanga vizuri ili mipango yetu hiyo ituongoze kufanya maamuzi sahihi na ya kimkakati. Inawezekana, tutekeleze wajibu wetu!

58. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo ninaomba sasa Kamati yako ipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25.

Mungu Ibariki Tanzania; Mungu Ibariki Afrika

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja!.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.
Jumatatu, 06 Novemba 2023

Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji,
1 Mtaa wa Ardhi,
S.L.P 104, 40403 Dodoma.